

Akoro ni mumewe Chichi. Wanaishi katika kijiji kiitwacho Kanam katika Kaunti ya Turkana.

Akoro ana bustani ya ndizi inayompatia mazao mazuri.




Siku moja kabla jua  
kuwa kali, Akoro  
aliondoka akibeba  
kreti ya ndizi mbivu  
kichwani kwake.

Alitembea kwa ujasiri  
akielekea sokoni  
Kilindo, umbali wa  
kilomita moja kutoka  
nyumbani kwake.



Wanaume na  
wanawake wa umri  
wake walimtazama  
kwa mshangao. Baadhi  
yao hata walimcheka  
kwa sauti, "Bila shaka  
Akoro amerogwa.  
Anawezaje kufanya  
kazi kama hii?  
Wanaume kutoka jamii  
yetu hawauzi ndizi!"

Lakini, Akoro hakujali.  
Alikuwa ameamua  
kuifanya kazi yoyote  
kwa bidii.



Alipowasili sokoni tu,  
Akoro alizipanga ndizi  
zake kisha akaketi  
karibu nazo akisubiri  
wateja.

Alijiuliza, “Kuna yeote  
atakayezinunua ndizi  
zangu?”



Dakika chache baadaye, mwanamke aliyevalia rinda la kizambarau, alikikaribia kibanda cha Akoro. “Unauza ndizi kilo moja pesa ngapi?” mwanamke yule aliuliza.

“Shilingi hamsini, dadangu,” Akoro alimjibu kwa heshima.



Mwanamke yule akasema, "Tafadhalini fungie kilo moja na nusu. Lakini, lazima unipunguzie bei."

Akoro akamjibu, "Hakuna shida dadangu, nitapunguza shilingi kumi. Wewe ni mteja wangu wa kwanza." Akoro alimpatia mwanamke yule ndizi zake.



Akoro alianza kufurahia biashara yake. Wanunuzi walivutiwa na ndizi zilizopendeza na maneno ya Akoro matamu.



Adhuhuri, Akoro alikuwa amechoka kusimama. Alikikalia kigoda akaendelea kuuza ndizi zake. Mwanamke aliyevalia rinda la bluu, alinunua ndizi nyingi.

Waliomcheka Akoro, walianza kushangaa jinsi biashara yake ya ndizi ilivyawiri.



Saa tisa alasiri, Akoro alimuuzia mwanamke aliyekuwa akitoka kazi ndizi zake za mwisho.

Aliwapa ndizi mbili mbili wanaume walioketi naye wakati huo wote.  
Walimtumbuiza kwa hadithi tamu alipowasubiri wateja.



Akoro alliondoka na  
kreti tupu kichwani.  
Alitembea akiimba  
wimbo wa furaha  
akijivunia kazi  
aliyoifanya siku hiyo.

Aliwaza, “Kufanya bidii  
kwa dhati ni jambo  
muhimu maishani.”



Aliinunulia familiia  
yake unga wa mahindi,  
mafuta ya mboga,  
chai, sukari na mkate.

Kisha alienda  
nyumbani kwa furaha.  
Mawazo yake yalijaa  
mipango ya kuipanua  
biashara yake ya ndizi.

